

Karibu tujifunze biblia.

Matendo 3:22 “Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi.

23 Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiliza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake”

Unabii huo unamhusu Bwana Yesu Kristo, lakini swali la Msingi hapa, je! Ni wakati gani ambao “watu wataangamizwa na kutengwa” kwa kutomsikiliza huyu Masihi...Kwasababu ni wengi leo hawamsikilizi wala kumtii lakini hawaangamizwi wala kutengwa na watu wao.

Hapo kuna mambo mawili ambayo yatatimia kwa pamoja.. **1)**

KUANGAMIZWA, na 2) KUTENGWA.

Haya ni mambo mawili ambayo yatatimia kwa wakati mmoja kwa wote ambao hawatamsikiliza Masihi.

Sasa swali, ni hili unabii huo utatimia lini wa watu kuangamizwa na kutengwa?

Tusome,

2 Wathesalonike 1:7 “na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; WAKATI WA KUFUNULIWA KWAKE BWANA YESU kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake

8 katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu;

9 watakaoadhibiwa kwa MAANGAMIZI ya milele, KUTENGWA na uso wa Bwana na UTUKUFU WA NGUVU ZAKE;”

Umeona hapo?. Kumbe wote wasioitii injili, leo siku ya mwisho (ya kufunuliwa Bwana Yesu) wataangamizwa!, na sio tu kuangamizwa, bali pia **“watatengwa na uso wa Mungu”** na **“kutengwa na utukufu wa nguvu zake”**...Maana yake wataanza kwa kutengwa kutoka kwa ndugu zao (*wakati wa kutenganishwa kondoo na mbuzi Mathayo 25:31-35*) na pia watatengwa na vitu vyote Mungu alivyoviumba ikiwemo dunia na kila kitu...sawasawa na Mithali 2:21-22.

Mithali 2:21 “Maana wanyofu watacaa katika nchi, Na wakamilifu watadumu ndani yake.

22 Bali waovu watatengwa na nchi, Nao wafanyao hila watang’olewa”

Ni jambo bayaa sana kutengwa na uso wa Mungu na kuangamizwa!..
Wengi leo wanamkataa Yesu na kuikataa Injili wakidhani ipo njia
nyingine ya kufika mbinguni.. Bwana Yesu yeye mwenyewe alisema kwa
kinywa chake kuwa..

Yohana 14:6 “..Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi”.

Hakuna njia nyingine ya kumfikisha mtu mbinguni isipokuwa njia ya Msalaba!.. Usidanganyike kwa vyovyyote vile.

Mwisho wa dunia unakuja, Mpokee Yesu leo, Itii injili yake inayosema...
usizini, usiibe, usivae mavazi ya nusu tupu, usivae mavazi yapasayo
jinsia nyingine, *usijichore mwili, usitukane n.k*

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

**Jiunge na kundi letu la mafundisho ya Biblia whatsapp kwa
kubofya hapa >> [WHATSSAPP-GROUP](#)**

Mada Nyinginezo:

**Je mwanamke anaruhusiwa kupanda madhabahuni akiwa katika
siku zake?**

**Ni kwa namna gani Kristo analitakasa kanisa kwa Maji katika
Neno? (Waefeso 5:26)**

Je Mungu ana njia ngapi za kuzungumza?

Wana wa Manabii walikuwa ni watu gani?

ATAANGAMIZWA NA KUTENGWA NA WATU WAKE.

REKEBISHA YAFUATAYO ILI UCHUMI WAKO UKAE SAWA.

Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp